# WAJIBU WA SERIKALI ZA MITAA KATIKA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

## Kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004

Mwandaaji: Fikiri Kenyela
Afisa Mazingira wa Manispaa
S.L.P 194
**MUSOMA**
Simu: +255 764 646 640/783 339 506
E-Mail: kenyelafs@yahoo.com

## Yaliyomo

Yaliyomo ... 2

1.0 Utangulizi ... 3

2.0 Mikataba ya Kimataifa ya Hifadhi ya Mazingira na Ushirikiano wa Kikanda ... 4

2.1 Mikataba ya Kimataifa ya hifadhi ya mazingira: ... 4

2.2 Ushirikiano wa Kikanda ... 5

2.3 Mashirika mbalimbali ya kimataifa kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira ni pamoja na: ... 5

2.4 Masuala ya mazingira yamepewa mkazo mkubwa katika mashirika na mashirikisho mbalimbali duniani ikiwemo; ... 7

3.0 TANZANIA ILIVYOJIPANGA KATIKA KUSIMAMIA UHIFADHI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA ... 7

4.0 Sera na Sheria kuhusu masuala ya Mazingira ... 7

4.3 Baadhi ya Kanuni (Principles) za Msingi zilizopo katika sheria ya uhifadhi wa Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004 ... 9

5.2 Kamati za Kudumu za Mamlaka za Serikali za Mitaa ... 14

5.3 Kamati za Kudumu za Miji, Kata, Vijiji na Vitongoji ... 14

5.4 Uteuzi wa Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji ... 15

5.4 Kazi za Ofisa Msimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji ... 15

5.5 Madaraka ya jumla ya Kamati za Usimamizi wa Mazingira za Jiji, Manispaa, Wilaya, Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji: ... 15

5.0 Hitimisho ... 16

6.0 Ushauri ... 16

## 1.0 Utangulizi

Mazingira maana yake ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka binadamu pamoja na yeye mwenyewe, viumbe vyenye uhai na visivyo na uhai, vya asili na visivyo vya asili na jinsi vinavyotegemeana.

Mazingira ni ghala la kuhifadhi malighafi zote zinazohitajika kuendeleza uhai wa viumbe hai na mfumo-ikolojia. Binadamu ni sehemu ndogo sana ya mazingira. Mahitaji yote ya binadamu hutunzwa ndani ya mazingira. Mazingira yanahusisha maumbile halisi yawazungukayo binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabianchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe, hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana.

Binadamu hawezi kuishi kama mazingira yatakoma kumpatia mahitaji yake kama maji, hewa, mwanga wa jua, chakula, udongo/ardhi, sehemu (space), nishati, na mahitaji mengine. Lakini mazingira yataendelea kustawi vizuri zaidi kama binadamu atakoma kuwa sehemu ya mazingira (Man cannot live without the environment but the environment can thrive without man).

Kwa bahati mbaya sana binadamu kama mshirika tu wa mfumo ikolojia katika mazingira amegeuka kuwa mharibifu mkubwa wa mazingira kuliko kiumbe mwingine yeyote. Kwa hakika shughuli za binadamu hususan za kiuchumi na kijamii ndizo chanzo kikubwa zaidi cha uharibifu wa mazingira. Mojawapo ya matokeo hatarishi ya uharibifu huo ni kupotea kwa uoto wa asili (deforestation), kuongezeka kwa hali ya jangwa (desertification), kuongezeka kwa joto duniani (global warming) kunakosababisha mabadiliko ya tabia nchi (climate change), kupungua kwa bioanuai (loss of biodiversity), kutoweka kwa viumbehai (extinction), kutoboka kwa tabaka la ozone, kuharibika kwa udongo/ardhi (land degradation) na mengine mengi. Binadamu anawanyima haki ya msingi ya kuishi katika mazingira bora viumbe wenzake na hata binadamu wenzake katika vizazi vijavyo (Inter generational Equity).

Kwa vile ni lazima mazingira yampatie binadamu mahitaji yake yote katika kufanya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, zana ya maendeleo endelevu (Sustainable development) ndiyo pekee itasaidia kuwezesha kupatikana kwa mahitaji haya kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Maendeleo endelevu maana yake ni maendeleo yenye kukidhi mahitaji ya kizazi kilichopo pasipo kukwamisha upatikanaji wa mahitaji ya vizazi vijavyo.

Kwa sababu hiyo sera, sheria, kanuni na miongozo imewekwa kwa lengo la kuingilia kati uharibifu wa mazingira unaofanywa na binadamu ili kuupunguza au kuuzuia kabisa. Lengo ni kuhakikisha kuwa hali ya mazingira inaendelea kuruhusu uhai wa viumbe hai katika dunia uendelee kuwepo na kufanya viumbe wa aina mbalimbali akiwemo binadamu kuishi katika mazingira salama ikizingatiwa kuwa viumbe wote wanaishi kwa kutegemeana sana kati yao

wenyewe na kati yao na viumbe visivyo na uhai kama vile hewa, maji, viini lishe, udongo, miamba, jua, halijoto, mwanga kwa kutaja kwa uchache.

Mikataba na sheria za kimataifa, kikanda, kitaifa na mamlaka za serikali za mitaa zihusuzo ulinzi wa mazingira zimewekwa kwa lengo hilo.

## 2.0 Mikataba ya Kimataifa ya Hifadhi ya Mazingira na Ushirikiano wa Kikanda

### 2.1 Mikataba ya Kimataifa ya hifadhi ya mazingira:

Kwa kuzingatia kuwa masuala ya mazingira hayajui mipaka ya mataifa yetu, nchi za dunia zimeweza kujiwekea mikataba mbalimbali ya kulinda mazingira. Maliasili nyingi zinavuka mipaka ya nchi moja hadi nyingine kwa mfano hewa katika anga; maji ya bahari, mito na maziwa; milima; misitu na wanyama wanaohamahama (migratory species). Mikataba ya kimataifa (multilateral agreements) na nchi mbili (bi-lateral treats) imeweza kuwekwa.

Tanzania ni nchi mwanachama wa Mikataba mbalimbali ya Hifadhi ya Mazingira. Lengo la kuridhia Mikataba hii ni kushirikiana na jumuiya za kimataifa katika kusimamia masuala ya kimataifa ya mazingira. Aidha, Tanzania imehuisha malengo ya Mikataba hii katika sheria za nchi ili kufanikisha utekelezaji wa Mikataba hii katika ngazi ya kitaifa. Mikataba hii inajumuisha;

1. Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai, Nairobi, (Convention on Biological Diversity (CBD)). Serikali ya Tanzania ilisaini Mkataba huu mwaka 1992 na kuridhia mwaka 1996.
2. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (UNCCD), 1994
3. Mkataba wa Basel wa mwaka 1989 kuhusu Udhibiti wa Usafirishaji wa Taka zenye Sumu baini ya nchi na nchi. Serikali ya Tanzania ilisaini mkataba huu mwaka 1993.
4. Mkataba wa Bamako kuhusu Uzuiaji wa Uingizaji wa Taka zenye Sumu Barani Afrika,1990;
5. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), 1992; Tanzania iliridhia mkataba huu mwaka 1996.
6. Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Wanyama walioko hatarini kutoweka kutokana na Biashara Haramu (CITES), 1973;
7. Itifaki ya Kyoto ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, 1997; Mkataba wa Kyoto kuhusu kupunguza gesijoto yaani hewa zinazosababisha kuongezeka kwa joto Duniani (greenhouse gas emission reductions) hususan hewa ya ukaa ili kupambana na mabadiliko ya Tabianchi. Tanzania iliridhia mkataba mdogo wa Kyoto mwaka 2002. Mkataba huu unalenga kuunganisha juhudi za jumuiya za kimataifa katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kujenga uwezo wa mataifa na jamii kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

8. Mkataba wa Vienna kuhusu Kulinda Tabaka la Hewa ya Ozoni, 1985;
9. Itifaki ya Montreal ya Kukabiliana na Kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni, 1987;
10. Itifaki ya SADC ya Hifadhi ya Wanyamapori na Utekelezaji wa Sheria, 1999;
11. Mkataba wa Urithi wa Dunia, 1972;
12. Makubaliano ya Lusaka ya Ushirikiano wa Utekelezaji majukumu ya Sheria dhidi ya Biashara haramu ya Wanyamapori na Mimea, 1994;
13. Mkataba wa Kuhifadhi, Kusimamia, na Kuendeleza Mazingira ya Bahari na Ukanda wa pwani wa nchi za Mashariki ya Afrika, 1985;
14. Mkataba wa Born wa Kuhifadhi Mazingira na Viumbe Wahamao (CMS), 1985;
15. Mkataba wa Ramsar wa kuhifadhi Ardhi-oevu, 1971;
16. Makubaliano ya Kuhifadhi Ndege wahamao wanaopendelea mazingira ya majini (AEWA), 1999;
17. Mkataba wa Kuhifadhi Ziwa Tanganyika na Bonde lake, 2003;
18. Mkataba wa Rotterdam kuhusu Taratibu za Taarifa za awali kuhusu Biashara ya Kemikali za Sumu na Viuatilifu,1998;
19. Mkataba wa kudhibiti Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa muda mrefu (POPs), 2001;
20. Itifaki ya Cartagena kuhusu Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa, 2000;
21. Mkataba wa Afrika wa Kuhifadhi Mazingira Asili na Maliasili, 1968; na
22. Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Sheria za Bahari, 1982.

## 2.2 Ushirikiano wa Kikanda

Tanzania ni mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kikanda ambazo pamoja na mashirikiano mengine, masuala ya mazingira yanapewa kipaumbele. Jumuiya hizo ni pamoja na:

1. Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (Southern Africa Development Community-SADC);
2. Jumuiya ya Afrika Mashariki (East Africa Comunity- EAC);
3. Umoja wa Afrika (African Union -AU); na
4. Ushirikiano wa nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi (Indian Ocean Rim-Association for Regional Cooperation- IOR-ARC).

## 2.3 Mashirika mbalimbali ya kimataifa kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira ni pamoja na:

1. United Nations Environment Programme (UNEP)
2. Earth System Governance Project (ESGP)
3. Global Environment Facility (GEF)

4. Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)
5. International Union for Conservation of Nature (IUCN)
6. World Nature Organization (WNO)
7. Centre for Science and Environment (CSE)
8. Wetlands International
9. Wildlife Conservation Society
10. Wolf Preservation Foundation (WPF)
11. World Business Council for Sustainable Development
12. World Conservation Union (WCU)
13. World Land Trust (WLT)
14. World Meteorological Organization (WMO)
15. World Resources Institute (WRI)
16. World Union for Protection of Life (WUPL)
17. World Wide Fund for Nature (WWF)
18. Deep Green Resistance
19. Earth Charter Initiative
20. Earth Day Network
21. Earth watch
22. Environmental Defense Fund
23. Fauna and Flora International
24. Forest Stewardship Council
25. Forests and the European Union Resource Network (FERN)
26. Friends of Nature
27. Friends of the Earth
28. Gaia Mater (the mother Earth)

Taarifa kamili kuhusu mashirika haya pamoja na miradi/shughuli yanazofanya zinapatikana kwenye tovuti: https://en.wikipedia.org/wiki/List_of_environmental_organizations.

**2.4 Masuala ya mazingira yamepewa mkazo mkubwa katika mashirika na mashirikisho mbalimbali duniani ikiwemo;**

1. Umoja wa mataifa (UN)
2. European Union (EU)
3. Umoja wa Afrika (AU)
4. Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)
5. Benki ya Dunia (WB)
6. African Development Bank (ADB)
7. SADC

## 3.0 TANZANIA ILIVYOJIPANGA KATIKA KUSIMAMIA UHIFADHI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Vuguvugu la umuhimu wa kuhifadhi, kulinda na kusimamia kikamilifu utunzaji wa mazingira na matumizi ya rasilimali mbalimbali duniani limekuwa hai sana katika miaka ya karibuni hasa miaka ya 1990 na kuendelea. Vuguvugu hili ulimwenguni mwote lilianza tangu miaka ya 1970 hasa baada ya mkutano mkubwa wa Umoja wa Mataifa uliohusu mazingira na makazi ya watu huko Sweden mwaka 1972 katika mji wa Stockholm. Mkutano huo ulitoa tamko rasmi (Stockholm Declaration) lililosisitiza pamoja na mambo mengine umuhimu wa kuhifadhi mazingira ya mwanadamu ambayo ni chanzo kikubwa cha uhai wake. Miaka ishirini baadae, (mwaka 1992) Mkutano mwingine wa kilele ulifanyika huko Rio de Jeneiro (Brazili) ambao pia uliweka changamoto kubwa katika suala zima la ulinzi, usimamizi na utumiaji endelevu wa mazingira na rasilimali tulizonazo.

Idara ya Mazingira ilianzishwa mwaka 1992 katika Wizara ya Maliasili na Utalii na kuunda Wizara ya Maliasili, Utalii na Mazingira. Kuanzishwa kwa idara ya mazingira kulitokana na juhudi za serikali katika kuhimiza utuzaji wa mazingira nchini kama ilivyohimizwa na Azimio la Rio mwaka 1992. Azimio la Rio (Rio-declaration) liliafikiwa na wakuu wa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa  Mjini Rio de Janeiro, Brazil. Azimio hili linazitaka nchi zote duniani kutambua uhusiano uliopo kati ya maendeleo na mazingira. Katika mkutano huo, Tanzania iliwakilishwa na Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Pili. Mnamo mwaka 1995, Idara ilihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ajili ya kutoa kipaumbele na kuipa nguvu kiutendaji katika masuala ya usimamizi wa Mazingira.

## 4.0 Sera na Sheria kuhusu masuala ya Mazingira

**4.1 Sera mbalimbali zinahimiza masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.**
Utunzaji wa Mazingira ni suala mtambuka, linapaswa kuonekana likitiliwa mkazo katika sera za sekta mbalimbali. Miongoni mwa Sera hzo ni:-

1. Sera ya Taifa ya Mazingira (1997);
2. Sera ya Kilimo na Mifugo (1997);
3. Sera ya Maendeleo ya Mifugo (2006);
4. Sera ya Sekta ya Uvuvi (1997);
5. Sera ya Misitu (1998); Sera Ufugaji Nyuki (1998);
6. Sera ya Wanyamapori (2007);
7. Sera ya Taifa ya Utalii (1999);
8. Sera ya Taifa ya Ardhi (1995);
9. Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu (1992);
10. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi (2000);
11. Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996);
12. Sera ya Taifa ya Maji (2002);
13. Sera ya Taifa ya Umwagiliaji (2010);
14. Sera ya Taifa ya Afya (2007);
15. Sera ya Taifa ya Nishati (2003);
16. Sera ya Madini (2009);
17. Sera ya Taifa ya Kukuza Uwekezaji (1996);
18. Sera ya Elimu na Mafunzo (2005);
19. Sera ya Taifa ya Usafirishaji (2003);
20. Sera ya Taifa ya Utafiti (2010);
21. Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000);
22. Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996);
23. Sera ya Usimamizi wa Majanga (1990);
24. Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (2003);
25. Sera ya Taifa ya Mashirika yasiyo ya Serikali (2002);
26. Sera ya Taifa Bioteknolojia (2010);
27. Sera ya Tasnia ya Ujenzi (2003); na
28. Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025).

### 4.2 Sheria mbalimbali zinahusika na usimamizi na hifadhi ya mazingira nchini

Baadhi ya Sheria hizo ni pamoja na:

1. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya mwaka 2004;
2. Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009;
3. Sheria ya Hifadhi na maeneo Tengefu ya Bahari Na. 29 ya mwaka 1994;
4. Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya 2003;
5. Sheria ya Misitu Na. 7 ya 2002;
6. Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali ya vyakula vya Mifugo Na. 13 ya 2010;
7. Sheria ya Mbolea Na. 9 ya 2009;
8. Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Kemikali Viwandani Na. 3 ya 2003;
9. Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya 2009;
10. Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi Na. 12 ya 2009;

11. Sheria ya Utalii Na. 29 ya 2008;
12. Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008;
13. Sheria ya Mafuta na Petroli ya Mwaka 2008,
14. Sheria ya Ufugaji wa Nyuki Na. 15 ya 2002;
15. Sheria ya Madini Na. 14 ya 2010;
16. Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999;
17. Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999;
18. Sheria ya Afya ya Jamii Na. 1 ya 2009;
19. Sheria ya Usalama na Afya Kazini Na. 5 ya 2003;
20. Sheria ya Kulinda Mimea Na. 13 ya 1997;
21. Sheria ya Usafirishaji Majini Na. 21 ya 2003;
22. Sheria ya Nishati Vijijini Na. 8 ya 2005;
23. Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya 2007;
24. Sheria ya Barabara Na. 13 ya 2007;
25. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Na. 8 ya 1982; na
26. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 ya 1982.

## 4.2 Kanuni na Viwango (Regulations and Standards) Zinazotumika katika Usimamizi wa Mazingira

Kanuni hizo ni pamoja na:

1. Kanuni ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Uperembaji (EIA and Audit Regulations), 2005
2. Kanuni ya Usajili wa Wataalamu wa Mazingira (Registration of Environmental Experts Regulations), 2005
3. Kanuni ya Viwango vya Ubora wa Hewa (Air Quality Standards Regulations), 2007
4. Kanuni ya Viwango vya Ubora wa Udongo (Soil Quality Standards Regulations), 2007
5. Kanuni ya Viwango vya Ubora wa Maji (Water Quality Standards Regulations), 2007
6. Kanuni ya Viwango wa Udhibiti wa Taka hatarishi (Hazardous Waste Control and Management Standards Regulations), 2009
7. Kanuni ya Viwango vya Usimamizi wa Taka ngumu (Solid Waste Management Regulations), 2009

## 4.3 Baadhi ya Kanuni (Principles) za Msingi zilizopo katika sheria ya uhifadhi wa Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004

Miongoni mwa kanuni hizo ni; **kanuni ya mchafuzi kulipa (Polluter pays principle)**. Sheria hii ya uhifadhi wa Mazingira inatamka wazi kuwa yeyote yule atakayebainika kuchafua mazingira analazimika kulipa kwa kiwango kile cha uchafuzi alioufanya. Lengo la hii kanuni ni

kuhakikisha kuwa mlipaji wa uchafuzi wa mazingira kwanza aogope kuchafua tena mazingira na pili uchafuzi uliofanywa unasawazishwa na ulipajihuo.

Kanuni ya pili ni ile ya **mtuhumiwa wa uchafuaji wa mazingira kuthibitisha mahakanani kuwa hachafui mazingira**. Hii ni kanuni ambayo iko tofauti na sheria nyingine zote ambazo humtaka yule anayemtuhumu mwenzake kuwa amefanya jambo fulani kinyume na sheria fulani kuithibitishia mahakama kuwa kweli mtuhumiwa amefanya vile. Sheria hii ya uhifadhi wa mazingira inatamka wazi kuwa mtuhumiwa wa uchafuzi wa mazingira anatakiwa athibitishe kuwa hachafui mazingira kama inavyodaiwa na mshitaki.

Kanuni ya tatu ni ile **ya ushirikishwaji wa wananchi katika kutathimini athari za kimazingira** katika mradi wowote ule unaotarajiwa kuanzishwa katika eneo fulani. Sheria hii ya uhifadhi wa mazingira inataka ushiriki wa wananchi wa eneo tarajiwa la mradi kuhusishwa moja kwa moja katika hatua zote za kutathimini athari za kimazingira zitakazoletwa na uanzishwaji wa mradi unao tarajiwa kuanzishwa.

Kitu cha msingi cha kukumbuka hapa ni kuwa mradi wowote ule unakatazwa na sheria hii kuanzishwa kabla ya kufanyiwa tathimini ya kina ya athari za kimazingira zitakazotokana na uanzishwaji wa mradi katika eneo Fulani. Ni ukiukwaji wa sheria hii, tena wa makusudi na uliodhahiri kuanzishwa mradi wowote ule nchini Tanzania bila ya ufanywaji wa tathimini ya athari za kimazingira wa kina na wenye ushirikishwaji wa wananchi wa eneo la mradi tarajiwa.

**Kanuni ya uchukuaji wa tahadhari (Precautionary principal)**. Sheria ya uhifadhi wa mazingira imejikita zaidi katika kuhakikisha kuwa uchafuzi wa mazingira hakutokei kabisa na siyo vinginevyo. Msingi mkubwa wa kanuni hii ni kuzuia kuharibika kwa mazingira kwa kufuata msemo wa Kiswahili wa “kinga ni bora kuliko tiba”. Hivyo basi sheria hii inachukua tahadhari na kuhakikisha kuwa uchafuzi hautokei kwa kuwa ukishatokea ni vigumu au haiwezekani kabisa kurudisha mazingira katika hali yake ya awali kabla ya uchafuzi huo kufanyika.

**Kanuni ya kuwa juu ya sheria nyingine**. Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira ya mwaka 2004, inasema wazi wazi kuwa pindi itakapotokea kuwa sheria yeyote ile inapingana na kipengele chochote cha sheria hii, basi kipengele au vipengele vya sheria ya Uhifadhi wa Mazingira 2004, kitatumika. Katika msingi huu ni wazi kuwa sheria ya mazingira itakuwa juu ya sheria zingine pindi utata utakapojitokeza. Sheria hii inaweka wazi kuwa katika mgongano au utata wowote


utakaojitokeza kimaantiki au kitaadhira, basi sheria ya uhifadhi wa Mazingira itumike katika kutoa utata huo. Kimsingi sheria ya uhifadhi wa mazingira ndiyo msingi wa kutatua utata / mgongano huo.

**Haki ya kupata habari za kimazingira:**
Ili mtu aweze kutimiza wajibu wake wa kutunza mazingira, kushiriki kikamilifu katika michakato na maamuzi yanayohusu mazingira ni lazima awe na uhakika wa kupata habari za mazingira ya sehemu na nchi yake, miradi inayofikiriwa kuanzishwa katika sehemu yake na mambo mbalimbali. Haki hii ni haki iliyotiliwa mkazo na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kuwa kila mtu ana haki ya kupata, kutafuta na kupewa habari. Haki hii haina kipingamizi au utofautisho wowote. Hivyo haishangazi kuona kwamba Sheria ya Mazingira, ya Mwaka 2004 inatambua na kutoa haki kwa kila raia kuwa, anayo haki ya kupewa habari na taarifa zilizoko katika mamlaka za umma zinazohusiana na mazingira, hali ya mazingira, hatari zilizopo na zinazoweza kujitokeza katika mazingira ikiwa ni pamoja na utoaji wa vichafuzi katika maji, hewa au ardhi, utupaji na umwagaji na utunzaji wa takamadhara.

## 4.4 Muundo wa kitaasisi wa utekelezaji wa sheria ya usimamizi wa mazingira namba 20 ya mwaka 2004

Utekelezaji wa masuala ya Mazingira umewekwa katika ngazi mbalimbali za kitaasisi. Katika kila ngazi kuna majukumu maalumu yanayotakiwa kutekelezwa. Ngazi ya juu kabisa ikiwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Makamu wa Rais (Waziri mwenye dhamana ya Mazingira), Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira, Mkurugenzi wa Mazingira, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Wizara za Kisekta, Sekretariet ya Mkoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Jedwali lifuatalo linatoa mchanganuo wa muundo wa kitaasisi katika kutekeleza sheria ya usimamizi wa mazingira namba 20 ya mwaka 2004.




Muundo wa Kitaasisi wa Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira

## 5.0 WAJIBU WA SERIKALI ZA MITAA KATIKA KUSIMAMIA MASUALA YA MAZINGIRA

Sheria ya Mazingira Na.20 ya mwaka 2004 imeweka bayana wajibu wa serikali za mitaa katika suala zima la kusimamia uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

### 5.1 Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Halmashauri

Fungu la 36 linasema;

(1) Kila Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Wilaya na Mji itateua au kuajiri Ofisa Usimamizi wa Mazingira ambaye atakuwa Ofisa wa umma na atakuwa;

(a) kwenye eneo la mamlaka ya Jiji, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Jiji;

(b) kwenye eneo la mamlaka ya Manispaa, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Manispaa;

(c) kwenye eneo la mamlaka ya Wilaya, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Wilaya; na

(d) kwenye eneo la mamlaka ya Mji, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Mji.

Kifungu cha (2) kinasema; Mtu aliyeteuliwa au kuajiriwa na Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Wilaya au Mji kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira atakuwa mwenye shahada au stashahada kutoka asasi ya elimu ya juu inayotambulika na mwenye uwezo katika usimamizi wa mazingira.

#### 5.1.1 Majukumu ya Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Halmashauri

Kifungu cha (3): Ofisa Usimamizi wa Mazingira atakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii kwenye eneo lake la kazi;

(b) kushauri Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya eneo lake la kazi kuhusu masuala yote ya mazingira;

(c) kukuza weledi kuhusu ulinzi wa mazingira na uhifadhi maliasili kwenye eneo lake;

(d) kukusanya na kusimamia taarifa kuhusu mazingira na matumizi ya maliasili kwenye eneo hilo;

(e) kuandaa taarifa za mihula kuhusu hali ya mazingira ndani ya eneo husika;

(f) kufuatilia maandalizi, mapitio na vibali vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) kwa ajili ya uwekezaji wa ndani;

(g) kufanya mapitio ya sheria ndogo zinazohusu usimamizi wa mazingira na shughuli maalumu za kisekta zinazohusiana na mazingira;

(h) kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu kuhusu utekelezaji wa Sheria; na

(i) kutekeleza majukumu mengine kwa kadiri mamlaka ya serikali za mitaa itakavyokuwa ikiyatoa.

## 5.2 Kamati za Kudumu za Mamlaka za Serikali za Mitaa

**Fungu la 37** (1) Kamati ya Kudumu ya Mipango Miji na Mazingira iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 42 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Masuala ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira iliyoazishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 74 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982, kila moja itakuwa Kamati ya Usimamizi wa mazingira ya Jiji, Manispaa au Wilaya kuhusiana na Jiji, Manispaa, na Wilaya kwa kila moja ya Kamati ya Kudumu iliyoanzishwa.

(2) Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Jiji, Manispaa na Wilaya itatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa chini ya vifungu vya (1) na (2) vya fungu la 55 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982 na kama itakavyokuwa, vifungu vya (1) na (2) vya fungu la 118 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 pamoja na kanuni zilizotengenezwa chini ya sheria hizo. (3) Bila kuathiri kifungu cha (2), Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Jiji, Manispaa na Wilaya pia- (a) itatekeleza kazi nyingine za ziada kama zilivyobainishwa na Sheria hii au kama, kwa nyakati mbalimbali, itakavyoagizwa na Waziri kwa Jiji, Manispaa au Wilaya kupitia taarifa iliyotangazwa kwenye *Gazeti la Serikali*; na (b) kutekeleza maagizo yoyote yaliyotolewa kwao na Waziri yanayohusu kuendeleza na kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira.

## 5.3 Kamati za Kudumu za Miji, Kata, Vijiji na Vitongoji

**Fungu 38** (1) Kila Kamati ya Kudumu ya Masuala ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya mji iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 96 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982, kamati maalumu iliyoundwa kufuatana na fungu la 107 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 pamoja na **Kamati ya Maendeleo ya Kata** iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 31 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982,yanayohusu eneo ilimoanzishwa Kamati hiyo- (a) itawajibika kusimamia mazingira kikamilifu yanayohusu eneo ilimoanzishwa; (b) itatekeleza kazi nyingine za ziada kama zilivyobainishwa na Sheria hii au kama itakavyoagizwa na Waziri au Baraza, kwa kila mmoja au mmojawapo; (c) itatekeleza maagizo yote yatakayotolewa kwake na Waziri yanayohusu kuendeleza na kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira; na (d) itatekeleza majukumu au kazi zingine zozote zinazohusiana na usimamizi unaofaa kwa

mazingira kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982.

(2) **Kamati ya Maendeleo ya Kijiji** ya kila kijiji itawajibika kusimamia kikamilifu mazingira kwenye eneo ilimoanzishwa na kwa utaratibu huo inaweza kufanya majukumu mengine yaliyotolewa chini ya ibara (a), (b), (c) na (d) za kifungu cha (1).

### 5.4 Uteuzi wa Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji

**Fungu la 39** linasema: Halmashauri ya Wilaya itamteua Ofisa wa umma kwa ajili ya kila eneo la utawala la mji, kata, kijiji, Mtaa na Kitongoji ambaye-

(a) kwenye eneo la mamlaka ya mji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mji;

(b) kwenye eneo la mamlaka ya Kitongoji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kitongoji;

(c) kwenye eneo la mamlaka ya Kata ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kata;

(d) kwenye eneo la mamlaka ya Mtaa ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mtaa; na

(e) kwenye eneo la mamlaka ya Kijiji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kijiji.

### 5.4 Kazi za Ofisa Msimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji

Fungu la 40 linaweka bayana kazi za Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji itakuwa ni kuratibu kazi zote na shughuli zinazolenga kuhifadhi mazingira kwenye eneo la mji, kata, mtaa, kijiji na kitongoji, au kadiri itakavyokuwa ndani ya Wilaya ya eneo husika.

## 5.5 Madaraka ya jumla ya Kamati za Usimamizi wa Mazingira za Jiji, Manispaa, Wilaya, Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji:

Kila Kamati ya Usimamizi wa Mazingira inayohusu eneo ilimoanzishwa, itakuwa na madaraka ya;

(a) kuanzisha uchunguzi na upelelezi kuhusu tuhuma yoyote inayohusu mazingira na utekelezaji au ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii;

(b) kumtaka mtu yeyote kutoa maelezo au taarifa kuhusu suala lolote linalohusu mazingira;

(c) kutatua migogoro kati ya watu binafsi, makampuni, wakala, asasi zisizokuwa za kiserikali, idara au asasi za Serikali, inayohusu majukumu, kazi, uwezo, wajibu au shughuli zao chini ya Sheria hii;

(d) kukagua na kuchunguza makazi, mtaa, gari, ndege au sehemu nyingine yoyote au kitu kinachoaminika au kuna sababu za msingi kuamini kuwa kichafuzi au vitu vingine vinavyoaminika kuwa vichafuzi vimewekwa au vinasafirishwa;

(e) kumtaka mtu yeyote aondoe kwa gharama yake, kitu au dutu yoyote kutoka mahali popote panapoaminika kuwa kitu au dutu hiyo inaweza kuhifadhiwa kwa usalama au kuharibiwa bila kuleta madhara kwa afya; na

(f) kufungua kesi za madai au jinai dhidi ya mtu yeyote, kampuni, wakala, idara au asasi inayoshindwaau kukataa kufuata agizo lolote lililotolewa na Kamati hizo.

## 5.0 Hitimisho

Kila mmoja wetu ni mdau muhimu sana katika kusimamia ulinzi na uhifadhi wa mazingira yetu. Sheria ya Mazingira ikizingatiwa ipasavyo, mazingira yetu yatatupatia mahitaji yetu yote na kubaki mahala salama pa viumbe kuishi, vizazi vya sasa na vile vitakavyofuata badala yetu. Binadamu analojukumu kubwa zaidi la kusimamia mazingira maana ndiye pia ni mharibifu mkubwa wa mazingira kuliko kiumbe mwingine yeyote yule kwenye mazingira. Tusimamie ulinzi wa mazingira ili mazingira yatutunze.

Baadhi ya changamoto za kimazingira katika halmashauri ya Manispaa ya Musoma ni pamoja na: 1. Uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira bado ni mdogo; 2. Kuwepo kwa shughuli za binadamu kama vile ujenzi na kilimo ndani ya mita 60 kutoka vyanzao vya maji (ziwa na mito); 3. Utiririshaji wa maji taka kwenye mitaro kutoka katika maeneo ya biashara, nyumba za kulala wageni, kambi na makazi; 4. Uchimbaji/Uchotaji wa mchanga kutoka ziwani hasa kata ya Makoko na Mwisenge; 5. Manispaa kutokuwa na dampo la kisasa (Sanitary Landfill) kwa ajili ya kutupa taka ngumu; 6. Utupaji wa maji taka bado ni kero ya kimazingira kwa vile hakuna mfumo wa kisasa wa kutibu majitaka kutoka mjini; 7. Kukosekana kwa usafiri kwa ajili ya kukagua na kufuatilia utunzaji na uhifadhi wa mazingira; 8. Mifugo kuzagaa onyo mitaani; 9.Kutokuwepo kwa bajeti kwa ajili ya usimamizi wa hifadhi ya mazingira; 10. Ukataji holela wa miti; 11. Athari za mabadiliko ya tabia nchi; 12. Uanzishaji wa miradi bila kuzingatia kanuni na sheria za mazingira, 13. Uvuvi haramu; 14. Uchafuzi wa hewa; 15. Muji kutokuwa na vivutio kama vile bustani nzuri. 16. Mfumo duni wa ukusanyaji, utunzaji, usafirishaji na utupaji wa taka ngumu (uhaba wa vifaa vya kutunzia taka mtaani (public literbins), magari n.k).

## 6.0 Ushauri

Ili kuboresha uhifadhi na usimamizi bora wa mazingira kwa jamii ya Musoma, ni vyema mambo yafuatayo yakafanyiwa kazi

1. Kutoa elimu ya mazingira kwa jamii ili kukuza weledi wa kutunza mazingira
2. Kukomesha shughuli za binadamu kama vile kilimo, ujenzi na uchimbaji wa mchanga kwenye maeneo ya fukwe za ziwa na mito ndani ya mita sitini (60).
3. Kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na utiririshaji wa maji taka pamoja na gereji bubu na uoshaji magari ziwani na mtoni.

4. Kujenga dampo la kisasa (Sanitary landfill) na kuboresha mfumo wa usimamizi wa taka ngumu ikiwa ni pamoja na kununua magari ya taka, vifaa vya kuhifadhi taka mtaani (public litterbins).
5. Kujenga miundombinu ya kusafirisaha maji taka pamoja na miundombinu ya kutibu maji taka.
6. Kuijengea uwezo ofisi ya Maafisa Mazingira wa Manispaa kwa kuipa usafiri wa kudumu ili kuweza kufanya shughuli za ukaguzi wa mazingira kwa ufanisi zaidi.
7. Kuhakikisha kuna bajeti ya kutosha kuwezesha shughuli za kutunza mazingira zinafanikiwa.
8. Kuhimiza upandaji na utunzaji wa miti.
9. Kuhakikisha uzingatiaji wa sheria ya mazingira namba 20 ya mwaka 2004 hasa wakati wa kuanzisha na kutekeleza miradi mbalimbali.
10. Kusimika vyombo vya kuhifadhi taka kwa muda (public liter-bins) maeneo yote ya watu hasa kwenye masoko, minada, mialo, vituo vya mabasi na daladala, sokoni na kandokando ya barabara ili watu wavitumie kuhifadhi taka wanazozalisha ili kuepusha watu wasitupe taka ovyo.

Fikiri Kenyela
**Afisa Mazingira wa Manispaa**
**Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.**